

Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo, Accelarating Progress*

2018 - 2021

# MILELE ZANZIBAR FOUNDATION

## Ripoti ya Kuongeza Maendeleo

www.mzfn.org




Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo, Accelarating Progress*

Milele Zanzibar Foundation
Mbweni, P.O. BOX 933, Zanzibar
Simu: +255772229997,
Barua pepe: info@mzfn.org

**Kupata taarifa zaidi, tembelea:**
www.mzfn.org

@milelezanzibarfoundation

# UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI



**Yousuf L. Caires**
Mwanzilishi Mwenza & Mkurugenzi Mtendaji
Milele Zanzibar Foundation

Tufuate katika mitandao ya kijamii
Facebook, Instagram, na YouTube:
@MileleZanzibarFoundation

Milele Zanzibar Foundation
*Kuongeza Maendeleo, Accelarating Progress*

www.mzfn.org

## Mpendwa msomaji, mshirika na mdau,

Kwetu sisi hapa Milele Zanzibar Foundation (MZF) kutekeleza programu zenye viwango vya juu na vinavyoangazia mapana yanayomurika mabadiliko endelevu ya jamii zetu maskini ndio kiini na kitovu cha hamasa, msukumo, dira na azma yetu katika kuharakisha maendeleo. Tangu kuanzishwa kwetu mwaka 2014, tumeweza kukua na kutanuka na kuwa taasisi yenye hadhi kubwa na inayoaminika katika nyanja mbalimbali za maendeleo visiwani Zanzibar.

Kwa kutoa aidha misaada kwa asasi nyengine ama kwa sisi wenyewe kusimamia utekelezaji wa miradi moja kwa moja, tumeweza kupaa na kujikita kama taasisi ambayo hutoa huduma kwa ajili ya kubadilisha maisha ya jamii za wanyonge;wenye fursa chache waliopo Unguja na Pemba.

Kwa miaka kadhaa sasa, tumekuwa tukitoa huduma za msingi za kuziwezesha jamii zetu kiujuzi na nyenzo ikiwa ni daraja la kujenga jamii ambazo zilizoimarika katika usatwi wao wa Maisha. Usaidizi wetu huo umeziweka jamii mbalimbali za Zanzibar kuwa katika nafasi na mweleko mzuri kimaendeleo. Aidha, kutokana na uimara huu, kumetokea mabadiliko katika maisha ya watoto, vijana, wanawake na jamii mbalimbali, hasa zile za maeneo yenye watu wenye hali ya chini kupindukia kimaisha.

Kusudio letu ni kutekeleza mipango ya maendeleo kwa taratibu-endelevu zinawaunganisha jamii tangu mwanzo, na kwa namna hiyo tumeweza kufanikiwa kutumia mbinu tofauti katika kutoa usaidizi unaohitajika katika jamii. Mbinu hizi ni pamoja na kujengea watu uwezo, kujenga uhusiano wa kimkakati na uimarishaji wa taratibu na miundo iliyojikita kwenye hali halisi ya hapa Zanzibar.

Juhudi hizi zimeanza kuleta matokeo yanayoridhisha na tuliyopendelea kuyaona. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita 2018-2021, mipango yetu imefanikisha uwezeshaji wa kiuchumi na kijamii kwa mamia ya wanawake na familia zao, na hivyo kubadilisha maisha yao yakawa bora zaidi.

Hasa-hasa, mipango yetu imeleta mabadiliko mazuri na ambayo yanaonekana wazi kwenye mambo ambayo tumeyalenga, yaani, **maisha ya watu, elimu na afya.**

Kwa mfano, kwa **upande wa maisha ya watu,** misaada yetu imeboresha upatikanaji wa huduma za kifedha na mitaji pamoja na kuwajengea wanufaika wetu weledi wa utunzaji fedha ambao umewazesha kina mama kufanya shughuli zao ziwe za kibiashara zaidi na kukua vilevile ujasiriamali wao umekuwa na tija zaidi na kukuza mipango yao ya kibiashara. **Kwa upande wa elimu,** tumeona taratibu- jumuishi zetu zikitanuka hadi nje ya skuli ili kuwawezesha wanafunzi kujijengea uwezo wa kupata ajira na weledi wa stadi za maisha ambazo zitawanufaisha kimaisha na kimapato baada ya kumaliza skuli. Vilevile, **kwa upande wa afya,** jamii za kimaskini za vijijini zimeweza kupata huduma bora zaidi za kiafya, na hili ni kutokana na juhudi za zetu za kupambana na changamoto za utoaji wa huduma za matibabu. Na kubwa na muhimu zaidi, tunatambua kwamba miundombinu ina umuhimu mkubwa katika uwezeshaji wa wanajamii. Tunafarijika kuona kwamba uwekezaji wetu katika uimarishaji wa miundombinu ndani ya kipindi cha miaka saba [2014-2020] tukiwa Zanzibar umezaa matunda kwa kuleta maendeleo chanya.

Maendeleo haya ni pamoja na ufungukaji wa fursa za ukuzaji wa uchumi ndani ya jamii kutokana na kufanyika kwa miradi ya ujenzi wa barabara, kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za kiafya kutokana na uwekezaji katika miundo mbinu ya maji, ujenzi pamoja na uboreshaji wa vituo vya afya. Yote haya yameleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu na mazingira ya kusomea Visiwani Zanzibar.

Haya ambayo nimetangulia kuyasema ni masuala ya msingi ambayo yanatakiwa katika kusukuma mbele gurudumu la mabadiliko kwa watu wenye uhitaji mkubwa Visiwani Zanzibar. Kutokana na nia yetu kubwa ya kuunga mkono juhudi za maendeleo ya jamii ya wananchi wa Unguja na Pemba, Bodi ya Wakurugenzi, Utawala na Wafanyakazi wa MZF wataendelea kuimarisha ushirikiano na Serikali, washirika wetu na taasisi zenye mwelekeo kama wetu na wadau wengine katika kudumisha na kuimarisha yale ambayo tumeyafanikisha ili kuweko matokeo bora ya muda mrefu ujao.

Kauli-mbiu yetu, **"Kuharakisha maendeleo, huanza na wewe",** imetoa nafasi maalumu katika ripoti hii kwa wanajamii wanaonufaika na programu zetu kupaza sauti zao.Kwa namna ya pekee basi, utasikia sauti za watu kutoka Unguja Kaskazini hadi Kisiwa cha Kokota kule Pemba wakielezea ni kwa namna gani wamekuwa sehemu ya safari yetu ya kuibadilisha Zanzibar.

***Naamini utafurahia kuisoma taarifa hii!***

# YALIYOMO

## KUHUSU SISI

Maono, Dhima, Mbinu yetu na Mkakati Wetu......................................05
Kujenga Uimara toka Chini ..........................................................06

## UCHUMI JAMII


Kuibua Fursa kwa Wakulima wa Mwani Zanzibar ..................................08
Kutana na Shujaa wa Ukulima wa Mwani kwenye Bahari Kuu.................09
Ubia kwa Lengo la Kuharakisha Maendeleo...........................................10
Kuongeza Uwezo wa Vijana Kuajirika Kupitia Kilimo Endelevu...............11
Tunaunga Mkono Wajasiriamali Wanawake ...........................................12
Hatua za Kuimarisha Upatikanaji Maji Pemba.........................................13
Ambulensi ya Baharini Inavyookoa Maisha.............................................14

## ELIMU

KURUKA VIUNZI: Tupambana ili Wasichana Wasome Sayansi.............16
Kushadidia Elimu Bora Pemba ...........................................................18
Kampeni ya Kurudisha Watoto Skuli.......................................................19
Ushirikiano kwenye Elimu.....................................................................20

## AFYA YA JAMII

Kuboresha Huduma za Afya Zanzibar.....................................................22
Jitihada zetu za WASH Zaokoa Maisha....................................................24
Msaada kwa Ukarabati wa Vituo vya Afya...............................................25




www.mzfn.org

# KUHUSU SISI!

## Maono

Ni kuona umahiri, uhimilivu na uendelevu kwa jamii za vijijini katika visiwa vya Unguja na Pemba

## Dhima

Ni kuongeza maendeleo kwenye sekta za afya, elimu na fursa za ustawi maeneo ya vijijini na pembezoni kwa kutumia mbinu jumuishi na miradi endelevu

## Mbinu yetu

Tunahakikisha watu tunaofanya nao kazi na kuwasaidia wanatoka kwenye changamoto zao mbalimbali na kuweza kuhimili kwa kuwajengea uwezo kupitia mifumo iliyopo, kuwafungulia fursa, kuwajengea uwezo kwenye afya, elimu na ustawi wa maisha yao tukiweka msisitizo wa kufanya kazi kuanzia ngazi za chini.

## Mkakati Wetu

Mkakati wetu umejikita katika kuamini kwetu kwamba wananchi ambao tunafanya kazi ya kuwaunga mkono katika nyanja mbalimbali, ndio ambao wana dhima kubwa zaidi katika kuzikabili changamoto zilizo mbele yao, huku wakiungwa mkono nasi pamoja na washirika wao katika programu za kuwajengea uwezo.

Hivyo basi, programu zetu za maendeleo ya kijamii ambazo ni jumuishi na shirikishi zinalenga shehia 24 zilizopo Unguja na Pemba. Lengo letu kuu la mradi wetu ndani ya kipindi cha miaka mitatu limekuwa ni kuboresha maisha ya jamii ambazo zimelengwa na taasisi yetu.

Kinyume na miradi ya miaka ya nyuma ambayo kwayo usaidizi uliasisiwa, ukasanifiwa na kutekelezwa wenyewe, kila sekta ikiangalia tu matokeo yake yaliyotarajiwa, katika Mkakati huu wa 2020 kumekua na muingiliano mkubwa wa malengo, huku pakiangaliwa ni kwa vipi sekta zinabebana na kusaidiana. Badala ya kujikita kwenye utaratibu wa kisekta, programu ya M2020 imechukua utaratibu ambao unazingatia zaidi kumuimarisha mtu binafsi, mwalimu, mama, mwanafunzi au mkulima kama mtu kamili mwenye mahitaji tofauti.

# **Kujenga Uimara** kuanzia Chini

Tangu awali, tulitambua umuhimu wa kufanya kazi na uongozi wa ngazi zote Zanzibar, kuanzia Serikali Kuu hadi ngazi ya Shehia. Mkakati wa Milele 2020 una lengo mahsusi la kuunga mkono jitihada za jamii kuanzia ngazi za chini. Uungaji mkono wa miradi kwenye ngazi za chini katika ngazi ya Shehia umefanikiwa katika uhusishaji mkubwa wa wanajamii katika kuwezesha kupanga mipango-shirikishi kwa minajili ya kutoa huduma za afya, elimu na mahitaji ya watu.

Kutokana na utaratibu huu, shehia ambazo zimewezeshwa zimefanikisha utekelezaji wa malengo yao ya maendeleo ya mwaka 2021 kwa asilimia 60. Usaidizi waliopata ulikuwa ni pamoja na kuzijengea uwezo Kamati za Mashauriano za Shehia (Shehia Advisory Committees) ili zimudu kazi ya kupambana na vikwazo na kuchuka fursa za kuleta maendeleo na kuratibu kwa weledi mipango ya maendeleo kwa kushiriki katika kusimamia mipango ya kila robo mwaka.

Kujengea watu uwezo kumesaidia kufungua fursa ambazo huko nyuma hazikupewa umuhimu wa kutosha na Serikali na washirika wake wa Maendeleo. Kisiwani Pemba, kwa mfano, mabadiliko chanya katika sekta muhimu kama zile za maendeleo ya afya ya watu na elimu yanaonekana yakichanja mbuga katika shehia za Msuka Magharibi na Sizini.

**Matokeo na mabadiliko kama haya yameonekana pia kule Mtende, Wilaya ya Kusini-Unguja, Makangale iliyoko Wilaya ya Micheweni, Pemba, na Mbuyutende iliyopo Unguja Wilaya ya Kaskazini "A". Moja ya viashiria vya mafanikio ni ule ukweli kwamba, asilimia 90 ya hii Mipango ya Shehia imetekelezwa kwa pesa za Serikali au wanajamii wenyewe.**



Kituo cha afya kilichojengwa na wanajamii Pemba ©MZF

**Mwezeshaji-jamii katika shehia hizi mbili, Bw Abdalla Hamad, alikuwa na haya ya kusema:**

"Kutokana na kuijengea uwezo Kamati ya Mashauriano ya Shehia, jamii yetu imepiga hatua katika utoaji wa huduma kwa kujenga kituo cha afya kukarabati vyumba vya madarasa na kuchimba kisima cha maji."

"Aidha, tumeshuhudia kupungua kwa idadi ya vijana wasio na ajira. Vijana wetu sasa wanajiajiri wenyewe kufanya kilimo asilia, kisichotumia mbolea za kemikali (organic farming) na shule zinafanya vizuri na idadi ya wanafunzi wanaoachia masomo njiani imepungua."



Bw Abdalla Hamad
© MZF

# UCHUMI JAMII















Kilimo cha mwani Zanzibar
©MZF

# Kuibua **Fursa kwa Wakulima wa Mwani** Zanzibar

**Tumekuwa tukizisaidia jamii maskini Zanzibar kujipatia pesa kwa kutumia rasilimali zinazopatikana humu ndani Visiwani.**

Usaidizi huu unaelekezwa kwenye kilimo cha mwani ambacho kinatoa ajira kwa zaidi ya wananchi 18,000, na asilimia kubwa ya hao waliosaidiwa ni wanawake. Ijapokuwa kilimo kinashika nafasi ya tatu katika uzalishaji wa pato la taifa (GDP) wakulima wanakwazwa na changamoto mbalimbali. Hizi ni pamoja na mavuno haba kutokana na magonjwa ya mimea na bei ya chini ya mazao yao kwa sababu ya kiwango kidogo cha uongezwaji wa thamani kabla ya kupelekwa sokoni.

Ndani ya kipindi cha miaka mitatu iliyopita, tumetoa mafunzo juu ya mbinu za ulimaji wa mwani kwenye bahari kuu, tumetoa mafunzo kwa wakulima 215 juu ulimaji wa mwani aina ya cotonii wenye thamani kubwa. Pia tumewapa mbinu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwenye kilimo chao kwa lengo la kuwapa mbinu saidizi za kuogea na kujiokoa kwa wafugaji wa mwani bahari Kuu. Tulishirikiana na Mradi wa Panje, shirika lisilo la kiserikali ambalo lengo lake kuu ni kuhakikisha wakulima wa mwani wanakuwa salama. Kimsingi, hili lilifanyika kwa njia ya kutoa mafunzo ya kuogelea, stadi ambayo ni muhimu katika kupunguza uwezekano wa kuzama na kufa baharini.

Aidha, ili kuchangia utafiti na uboreshaji katika sekta ya uongezaji thamani kwenye sekta ya zao la mwani, tulianzisha Mradi wa Kiubunifu wa Mwani, Milele Innovation Park (MIP). Hadi kufikia sasa, MIP imebuni na kufanya majaribio kwa aina mbili za zao la mwani ambayo imeonyesha matokeo yanayoridhisha. Vilevile tuligawa pakiti 2500 za mbolea ya asili kwa wakulima wa mwani ili kukuza uzalishaji na kupanua soko la bidhaa za mwani.

# Kutana na **Shujaa wa Ukulima wa Mwani** kwenye maji marefu

Kaije Said Bakar, mama wa watoto sita kwenye Kijiji cha Tumbe, Pemba, ni mmoja wa wanufaika wa programu ya mafunzo ya kilimo cha mwani Bahari Kuu. Tayari Bi Kaije ameshakuwa mmoja wa waalimu waandamizi wawili tu kwenye eneo lao wenye sifa za kuendesha mafunzo ya kilimo cha mwani Bahari Kuu na uogeleaji wa kujiokoa.

Bi Kaije anajivunia kwa yale ambayo amefanya katika kuinua uwezo wa viwango vya uzalishaji wa wakulima wa mwani wenzake, hasa kina mama wa eneo analoishi;Tumbe. Anasema: "Nimetoa mafunzo kwa wakulima wapatao 140 hapa Tumbe, wakulima 30 wa Msuka, 30 wa Shumba Mjini, wanne Kojani na wengine wanne Chwale...Napata faraja kubwa ninaposaidia watu wa eneo ninaloishi na hata wale wa vijiji vya jirani."

Akielezea ni kwa kiwango gani ukulima bora wa wa mwani umemnufaisha, anasema: "Nina kila sababu ya kuwashukuru MZF kwa msaada wao ambao umetuwezesha kupata taratibu bora kabisa za kilimo na matokeo yake ni kwamba tunavuna zaidi na kuuza zaidi...Sina tatizo tena katika kuitimiza mahitaji ya watoto wangu sita kwa upande wa elimu, afya na elimu."

Aidha, tuliwawezesha wakazi wa Tumbe kujipanga katika vikundi vya kuweka akiba kwa kuunda jumuiya za vijiji za kuweka na kukopa (VSLAs) ili wawe na taratibu-endelevu za kupata fedha za kufanya shughuli za maendeleo. Miongoni wa vyama vya ushirika ambavyo vimeundwa na kusajiliwa ni kile cha Ushirika wa Ipo Sababu.

Katibu wake alikuwa na haya ya kusema: "Tunawashukuru MZF kwa kutuwezesha kujipanga kwenye kikundi cha watu 50. Hadi kufikia sasa, kikundi hiki kimefanikiwa kukusanya takribani Sh2.5 milioni kwa lengo la kuwasaidia wakulima ambao wanahitaji mikopo yenye masharti nafuu kwa minajili ya kufanikisha shughuli zao.

> **"Nimetoa mafunzo kwa wakulima wapatao 140 hapa Tumbe, wakulima 30 wa Msuka, 30 wa Shumba Mjini, wanne Kojani na wengine wanne Chwale"**

> **"Nina kila sababu ya kuwashukuru MZF kwa msaada wao ambao umetuwezesha kupata taratibu bora kabisa za kilimo na matokeo yake ni kwamba tunavuna zaidi na kuuza zaidi"**



**Kaije Said Bakar**
Mkufunzi mbobezii katika ukulima wa mwani kwenye bahari Kuu © MZF

# Ushirikiano kwa Lengo la Kuharakisha Maendeleo

Tunaamini kwamba kilimo Cha Asili kisichotumia mbolea za kemikali (organic farming) kinawezekana Zanzibar. Ni kwa sababu hiyo tangu mwaka 2019, tumekuwa kwenye mstari wa mbele katika mradi wa kilimo unaojulikana kwa jina la Harakati ya Kilimo  Asilia (Zanzibar Organic Initiative (ZOI)) ikishirikiana na washirika mbalimbali na wadau. Hawa ni pamoja na Zanzibar Spice Growers, Practical Permaculture Institute of Zanzibar, Umoja wa Wakulima wa Mbogamboga na Matunda Zanzibar (UWAMWIMA), Msonge Farm, Stone Youth Centre na One Farm.



**Ally Salim Jecha**
Mkulima wa kilimo kisichotumia kemikali
© MZF

Kama taasisi tumesaidia ZOI katika kuandaa mikutano ya robo mwaka na mikakati ya kutangaza shughuli zake kwa njia ya redio na televisheni. Kutokana na kuwepo kwa ushirikiano makini wa kimkakati kati ya sisi na Serikali, sasa hivi hakuna mkinzano wowote kati yetu na Serikali juu ya kilimo asilia na kumekuwa na mwamko wa juu wa swali hili miongoni mwa wananchi na wadau wa sekta binafsi.

Zaidi ya hayo, mpango huu umetoa usaidizi kwa wakulima kwa kutatua baadhi ya changamoto ambazo zimekuwa zikiwakwaza kama vile taratibu duni za kilimo, uhaba wa pembejeo, uhaba wa huduma za wataalamu wa kilimo na misaada ya kifedha na upatikanaji wa soko la mazao. Tumekuwa tukitumia mbinu za aina mbalimbali katika kuwasaidia wakulima wadogo-wadogo. Mbinu hizi zimekuwa pamoja na kuwajengea wakulima uwezo, kuwapanulia mtandao pamoja na kuwahamasisha. Tafiti zimeonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko la kipato kwa asilimia 15 miongoni mwa wakulima walioshiriki katika utafiti. La muhimu pia ni kwamba, uzalishaji umeongezeka kwa wastani wa kutoka asilimia 0.5 hadi 6.0.

Ally Salim Jecha ni mmoja wa wa wanufaika wa usaidizi wa MZF katika uendelezaji wa kilimo asilia, naye ana hili la kusema: "Nilianza kupata usaidizi wa MZF tangu mwaka 2019 baada ya kuelewa hasara za ukulima uliozoeleka wa kilimo kinachotumia mbolea za kemikali/viwandani. Ninawashukuru sana MZF ambao wameniwezesha kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya uwezeshaji yakiwa ni pamoja na yale ya uzalishaji wa mbegu bora za kisasa pale Morogoro, ambayo yaliandaliwa na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT). Kufuatia ujuzi niliopata, siku hizi siwapi tena watoto wangu chakula kilichozalishwa kwa kutumia mbolea ya kemikali na kwa sasa mimi ni gwiji wa kilimo cha mbolea asilia kwa ajili mahitaji ya familia na ya kibiashara." Bw Jecha ni mmiliki wa ekari nne za shamba ambalo udongo wake hurutubishwa kwa mbolea asilia pekee. Mazao anayopanda ni ndizi, mananasi, mapapai, pasheni, vitunguu, mimea ya dawa n.k. MZF imetilia mkazo kilimo cha mbolea asilia kwani, pamoja na kuwanufaisha wakulima wadogo-wadogo, vile vile ni kilimo kinachozalisha chakula ambacho ni bora kiafya. Aidha, aina hii ya kilimo ina tija zaidi kiuchumi na ni rafiki zaidi kwa mazingira kikilinganishwa na kile kilichozoeleka.

**"MZF tunaamini kilimo hai kinawezekana kwa 100% Zanzibar"**

# Kuongeza **Uwezo wa Vijana Kuajirika** Kupitia Kilimo Endelevu

Tunaunga mkono programu za kuwawezesha vijana kama mradi wa Fursa Kijani (Green Opportunity) kwa lengo la kuwapa vijana fursa ya kukua kimaslahi.

**Kupitia programu ya vijana ya Fursa Kijani, vijana wa Visiwani walifaidika kwa kupata stadi muhimu za maisha kupitia utaratibu wa kilimo-endelevu asilia. (permaculture).**

Matokeo ya utaratibu huu umesaidia kuongeza nafasi za ajira na fursa zaidi za ujasiriamali kwa vijana wa Zanzibar. Programu hii ina faida mbili kuu: ya kwanza ikiwa ile ya kuwapatia vijana ajira kwenye sekta ya kilimo na pili ni kuhamasisha shughuli za uzalishaji zinazotunza mazingira (green jobs). Aidha, programu iliwalenga pia vijana maskini wa Kizanzibari ambao walipata mafunzo ya stadi za maisha ambazo ziliongezwa nguvu na elimu waliyopata ya stadi za kilimo-endelevu asilia.

Programu ilifanikiwa kuwafikia vijana wapatao 100 ambao walipatiwa mafunzo juu ya stadi za kilimo-endelevu asilia, mwenendo mwema, na vitendo vya ujasiriamali ambao unatunza mazingira. Vijana wapatao 35 walipata ajira katika sekta ya kijani na wengine wakajiari wenyewe kwa kutumia stadi walizojifunza chini ya programu hii.

Zaidi ya hayo, programu hii ilishirikisha vyombo mabalimbali vya habari na kazi ya utetezi kwa lengo la kuamsha hamasa ya jamii juu ya masuala ya mazingira kwa ujumla na umuhimu wa kuekeza kwenye kilimo hai  kama njia mujjarrab ya kupambana na athari za tabia-nchi. Maeneo mengine yaliyoshughlikiwa katika programu hii yalikuwa ni pamoja na yale ya uharibifu wa mazingira na changamoto za afya, hasa za magonjwa yasiyo ya kuambukiza yatokanayo na lishe mbovu na matumizi makubwa ya mbolea za kemikali.

Tulitekeleza programu hii tukishirikiana na Practical Permaculture Institute of Zanzibar (PPIZ).



Moja ya mashamba asilia ya vijana waliowezeshwa Zanzibar © MZF


**100** Vijana 100 wamefikiwa na mradi huu

**35** wameajiriwa kwenye sekta ya kijani, wengine wamejiajiri

# **Tunaunga** Mkono **Wajasiriamali Wanawake**

Tangu mwanzoni kabisa, MZF na Umoja wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) ambayo ni mshirika wake kwenye kutekeleza mradi wa Kuwawezesha Wanawake (Women Empowerment (WEZA), walitambua kwamba ili kuboresha maisha ya wanawake maskini Visiwani Zanzibar, kujiingiza kwenye ujasiriamali ni mojawapo ya njia za uhakika.

**Hivyo basi, taasisi hizi mbili (MZF na TAMWA) ziliunganisha nguvu zao katika kutekeleza hatua za kuwezesha kiuchumi kina mama kwa kutumia mfumo wa vikundi vya kuweka na kukopa (VSLAs).**



**Wanawake**
**8,140**
**walifikiwa na programu hii katika vikundi 372**



**Bilioni 1.6+ Tsh**
**zilipatikana**



**programu ilikua Unguja vijijini na Pemba**

**Wilaya ya; Kusini, Kati, Kazikazini A na Kaskazini B.**

**Wilaya ya; Wete, Mkoani, ChakeChake na Micheweni.**

Programu hii ilitumia njia mbalimbali za kuwahamasisha kina mama wajiunge na Vikundi vya Kuweka na Kukopa (VSLAs) ili wajishughulishe na ujasiriamali kila mmoja kwa kikundi apendacho kama mtu binafsi au katika kikundi. Kulingana na muundo wa mradi, kina mama waliweza kujitungia kanuni na taratibu zao wenyewe ambazo ziliwapa mwongozo wa kuendesha shughuli zao na nidhamu inayostahili. Kwa mfano, mwongozo ulionyesha ni kiasi gani cha akiba mtu alipaswa ajiwekee na ni wapi aekeze.

Urahisi wa kujichagulia mnyororo wa thamani ulikuwa ni moja ya njia ambazo ziliiwezesha programu kufanikiwa. Hatimaye jumla ya takriban Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia 6 (1, 617,869,287) zilipatikana na wanawake wapatao 6,529 waliweza kujiingiza katika shughuli za ujasiriamali na kwa sasa wamekuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji yao binafsi na ya familia zao.

Mojawapo ya vikundi ambavyo vimenufaika na programu hii ni ushirika wa wajasiriamali wanawake wa Kijiji cha Bambi, Wilaya ya Kati,Unguja. Wanachama wa kikundi hiki walipata msaada wa mashine na jengo kwa ajili ya utengenezaji sabuni. Zeyana Seif Salim ni mmoja wa viongozi wa kikundi ambaye ana jukumu la kutoa mafunzo ya utengenezaji na uuzaji sabuni.

Anasema yafuatayo: "Tunatumia malighafi ambazo zinapatikana hapa hapa Zanzibar, kama vile mwani, karafuu na aloe vera. Hadi kufikia sasa, kituo cha ushirika huu una wanachama 25 na miongoni mwao, wawili ni wanaume. Ushirika huu unatumika pia kama kitovu cha mafunzo na tangu kuanzishwa kwake tayari kimeshatoa mafunzo kwa watu 265."

"Kwa wastani, ninapata laki 3 na nusu (Sh.350,000) kwa mwezi, kiasi ambacho kinasaidia sana katika kukidhi mahitaji ya familia yangu na ya watoto wangu watatu."



**Zeyana Seif Salum**
Mjasiriamali wa kutengeneza sabuni © MZF

# **Hatua za Kuimarisha** Upatikanaji Maji **Pemba**

Ni vigumu kufikiria maisha bila ya maji safi na ya kutosha, kwani inakuwa hali ambayo inayohatarisha afya za watu na kushusha ubora wa maisha katika jamii. Pamoja na ukweli huu, hali hii isiyofaa ndiyo iliyokuwepo kwenye Kisiwa Kidogo cha Kokota miaka nenda, miaka rudi. Kokota ni kimojawapo cha visiwa vidogo-vidogo vilivyo mkabala na Kisiwa cha Pemba. Kokota inakaliwa na wakazi zaidi ya 500.

Kunako mwaka 2019, tuliishirikiana na Mamlaka ya Maji ya Zanzibar (ZIWA), kuanzisha mradi wa maji kwenye kijisiwa hiki ulioitwa Kokota Water Initiative. Chini ya mradi huu, palitandazwa bomba kwa ajili ya kupitisha maji toka Mtambwe, Pemba, zikapitishiwa baharini hadi kwenye kijisiwa hicho.

Kabla ya uboreshaji wa upatikanaji wa maji, maisha pale Kokota yalijaa changamoto na hatari. Kiongozi mmoja katika eneo hili, Adam Khamis Khamis, anasema: "Maisha kwenye eneo letu yalikuwa magumu sana; wanakijiji walilazimika kutumia muda na rasilimali nyingi kwa minajili ya kwenda kutafuta maji, wakisafiri kwa vidau hadi Mtambwe, Pemba.

Anaongezea: "Tumejawa na furaha kwamba, kutokana na msaada wa MZF, sasa tunapata maji salama na safi. MZF pia pia ilisaidia katika kusimamisha matenki sita, kila moja likiwa la ujazo wa lita 5,000 kwa minajili ya kuhifadhia maji."



**Jabu Heri Makame,**
Mwanakijiji wa Kokota © MZF

Uhaba wa maji uliathiri vibaya wanakijiji wa Kokota, hasa wanawake. Jabu Heri Makame ambaye ni mama wa watoto wanane, anasimulia hali ilivyokuwa:

**"Tulikuwa tunalazimika kununua dumu la lita 20 kwa Sh300… sasa nyakati nyingine huwa nahitaji hadi lita 300 kwa siku, hasa pale ambapo tulipokua tunataka maji kwaajili ya kufulia nguo zetu. Tulilazimika kutumia hadi Sh9,000 kwa siku kwa ajili ya maji tu, kiasi ambacho ni kikubwa kupindukia kwa familia yenye kipato duni kama yangu! Changamoto hii iliathiri vibaya mno maisha yetu.**



Mwanafunzi akinywa maji safi ya bomba kijiji cha Kokota © MZF

# Ambulensi ya Baharini **Inavyookoa Maisha**

Wananchi wa Kisiwa cha Kokota, kama ilivyo kwa wananchi wa maeneo mengine ya nchi, walihitaji kupata huduma ya afya na matibabu pale ilipohitajika. Hata hivyo, hakuna hata kituo kimoja cha afya kwenye kisiwa hiki kwa hivyo, mkaazi wa Kokota anapokuwa na haja ya matibabu, hulazimika kusafirishwa hadi Hospitali ya Wilaya ya Wete.

Kwa vile hakuna boti za kisasa, wagonjwa, ikiwa ni pamoja na wanawake wajawazito na watoto, hubidi wasafirishwe kwenye mashua zilizoundwa kienyeji na ambazo usalama wake ni mdogo. Aidha, mashua hizo huchukua muda mwingi wa karibu masaa sita kutoka Kokota hadi Wete!



Ambulensi ya baharini iliyotolewa na MZF
© MZF

**Pili Mohamed Rashid ambaye ni mama wa watoto saba, anasimulia yaliyomsibu:**

"Nilikuwa mjamzito, sasa siku moja, nikaanza kupata maumivu ya uchungu. Mimi na wasaidizi wangu tukaondoka kwa miguu kuelekea pwani ili tupande boti nipelekwe Hospitali ya Wete. Baada ya kushuka bandarini ili tuelekee Wete, huku wasaidizi wangu wamenibeba, uchungu ulichachamaa, nikajifungulia njiani!"

**Hata hivyo, anasimulia mzazi huyu, alifikishwa hospitali na kitoto mikononi mwa mmoja wa ndugu zake.**

"mimi na mtoto tusalama na tunaendelea vizuri,"

**anamalizia kisa chake.**



**Pili Mohamed Rashid**
© MZF






# ELIMU





LET'S LEARN
English
for Zanzibar Primary Schools
Pupil's Book





# KURUKA VIUNZI:

# Kupambana ili Wasichana Wasome Sayansi

**Ikiwa kama sehemu ya lengo la kimkakati la MZF kuunga mkono elimu-jumuishi, taasisi hii ilishirikiana na Chuo Kikuu Cha Taifa (State Universty of Zanzibar (SUZA) na Forum for African Women Educationist (FAWE) kutekeleza programu ya miaka mitatu iliyopewa jina la STEM for Success in Zanzibar.**



Mwanafunzi akichunguza roboti kwa udadisi © MZF



Wanafunzi katika darasa la STEM © MZF Library

**Programu hii ilitumia mbinu-bunifu katika kusaidia wanafunzi, waalimu, skuli, taasisi za elimu na wataalamu wa elimu ili kuweka msukumo wa kuwa na mfumo sahihi wa kufundishia ambao utawezesha kuwe na uungwaji mkono wa hatua za kuleta uwiano mzuri kati ya wasichana na wavulana katika STEM—Sayansi, Teknolojia, Uinjinia na Hesabu—na wanafunzi husika wapate matokeo mazuri.**

Vilele, kwenye kiini cha programu hii, lengo kuu lilikuwa kuwafanya wasichana wapende kushiriki kwenye STEM. Kwa kuegemea kwenye uhusiano tuliojenga kati ya sisi na SUZA, tulitumia burudani na njia za kufurahisha katika kuwashirikisha wanafunzi kama vile kambi za STEM, mashindano ya kielimu kambi za mafunzo kwa lengo la kuboresha matokeo ya kielimu. Hili lilitekelezwa kama mradi, mtindo ambao uliwawezesha wanafunzi kuuona uhusiano kati ya yale waliyokuwa wakijifunza shuleni na yale yaliyomo katika mazingira wanayoishi.


'Katika kuratibu mafunzo, kila skuli ilikuwa na mwalimu wa STEM. Miongoni mwa waalimu hao ni Abbas Mohamed na Halima Abdulaziz kutoka Skuli ya Sekondari ya Mikindani.

Kuhusu programu hii, Bi Abdulaziz alikuwa na haya ya kusema: "Changamoto kubwa ilikuwa hii dhana kwamba mtoto wa kike hawezi kuyamudu na kufanya vyema masomo ya STEM, lakini hii ni dhana potofu na haina ukweli wowote kwa sababu sasa uzoefu unaonyesha wanafunzi wa kike na wa kiume, iwapo wamekuzwa pamoja na kupata usaidizi  sawa, wote wanakuwa na uwezo wa kufanya vizuri katika masomo ya STEM. Kwa mfano, katika programu hii, tumeona wasichana wakifanya vizuri kama wavulana, na mara nyingine wasichana walionyesha kufanya bora zaidi kuliko wavulana."

## Mwalimu Mohamed anasema:

"Ninafurahi kuwa mmoja wa watekelezaji wa programu ambayo iliundwa ili kuwasaidia wanafunzi wa kike kufanya vizuri katika STEM. Wakati wa kutekeleza mradi huu, nilikuwa nasimamia vilabu vya sayansi vya skuli yangu ambayo  tuna mabalozi wa wanafunzi watano (wasichana watatu na wavulana wawili).

"Wanafunzi na waalimu wetu walinufaika na kambi za mafunzo kwa kupata maarifa kwa njia ya vitendo, wakaelewa juu ya matumizi ya vifaa vya  kujifunzia na kufundishia sayansi ambavyo baadhi vimeundwa hapa-hapa Visiwani.Kambi zetu zilisaidia sana kuwajengea wanafunzi ubunifu na kuwapa stadi za maisha."




**Ndugu Abbas Mohamed**
Mwalimu katika skuli ya sekondari ya Mikindanil © MZF



Wanafunzi katika kipindi kwenye darasa la STEM ©MZF

## Hudhaima Salum Makame, mwanafunzi wa Kidato cha Nne, anazungumzia uzoefu alioupata kwenya mradi wa STEM ulioendeshwa na MZF wakishirikiana na FAWE na SUZA kwa kusema:

"Jambo moja ambalo kamwe sitalisahau ni kule kufungukiwa na kupata maarifa  ya uchaguzi wa kazi..Maarifa haya yameniwezesha kufikia uamuzi wa kazi ambayo ninaipenda kuisomea ambayo ni utabibu—Napenda siku moja niwe daktari."

## Anaongezea:

"Jambo ambalo nililipenda sana katika kambi lilikuwa majadiliano tuliyokuwa tunafanya kwenye vikundi, na mafunzo mbalimbali ya stadi za maisha ambayo yametujengea hali ya kujiamini kama wasichana."



**Hudhaima Salum Makame**
Mwanafunzi, skuli ya sekondari ya Mikindani © MZF

# **Kushadidia** Elimu Bora **Pemba**

Kwa kuzingatia kwamba walimu ndio wafundishaji ambao huwapa watoto elimu rasmi tangu wakiwa wadogo, tumefanya kazi na walimu Unguja na Pemba ili kuboresha uwezo wao wa kutoa elimu.

Jambo kubwa lililofanyika katika programu hii lilikuwa kuwajengea waalimu uwezo. Kwa mfano, chini ya mradi uliojulikana kama Promoting English Language and Literacy (PELL), walimu wa Pemba na Unguja walinufaika vilivyo. Msaada wetu pia uliwezesha kuandaa programu iliyojulikana kama 'Fun with English iliyowasaidia walimu kuongeza ujuzi wa kufundisha lugha ya kiingereza.

Bi Zuwena Ally Hamad ambaye ni mwalimu Skuli ya Msingi ya Minungwini, Wilaya ya Wete, Pemba, mmoja wa wanufaika wa programu ya PELL, ana haya ya kusema: "Mafunzo ya kujengea walimu uwezo yalikuwa muhimu sana kwani yametuongezea kujiamini katika ufundishaji darasani."

Mafunzo haya yametuongezea uwezo wa kuwasaidia wanafunzi wetu wajue namna bora ya kujifunza na kufikiri".Alisema Bi Zuwena.

**"Hali hii ni tofauti na ya miaka ya nyuma ambapo hatukuwa na uwezo wa kutumia vifaa vya kufundishia vilivyotengenezewa hapa hapa visiwani. Kutokana na utumiaji wa mbinu mpya za kufundishia, ufaulu wa wanafunzi wetu darasani umeongezeka."**

**Bi Zuwena Ally Hamad**
Mwalimu wa skuli ya msingi ya Minungwini



**Bi Zuwena Ally Hamad**
Mwalimu wa skuli ya msingi ya Minungwini ©MZF Library

# **Kampeni ya** Kurudisha Watoto Skuli

Pia tulitekeleza kampeni ya kuwarudisha na kuwabakisha darasani watoto waendelee na masomo. Watoto ambao huko nyuma walikuwa na tabia ya kutoroka skuli. Vile vile, tumewapa motisha wabaki skuli wale ambao walikuwa katika hatari ya kukatisha masomo. Aidha, pamoja na ujumbe wa kuwahamasisha watoto kwenda skuli, mradi huu pia uliwaunga watoto mkono kwa kuwagawia mabegi ya skuli. Wanafunzi wapatao 2,000 wa Shule ya Msingi ya Minungwini waligawiwa mabegi. Mmoja wa Watoto walionufaika na Kampeni hii, Mohamed Omari Mohamed ambaye yuko Darasa la 4, alikuwa na haya ya kusema:

**"Nilifurahia sana kupokea begi la skuli bila kudaiwa chochote, begi ambalo linaweza kubeba madftari saba. Hili linanimotisha nihudhurie skuli bila kukosa na maksi zangu kwenye majaribio zimeongezeka. Kwa mfano, mwaka huu nimepasi vizuri na kuwa miongoni mwa wanafunzi 10 bora kwenye darasa letu. Kwa hakika ninawashukuru sana MZF."**

Skuli ya Minungwini ina wanafunzi 2,094. Wastani wa vipato vya wakazi wa Minungwini ni vidogo mno kiasi kwamba, wengi wanashindwa kuwanunulia watoto wao mabegi ya skuli. Hivyo, wanafunzi wengi katika eneo hili walilazimika kutumia mabegi yaliyotengengenezwa kienyeji, na haya hayabebeki kwa urahisi.




**Mohamed Omari Mohamed**
Mwanafunzi wa skuli ya msingi Minungwini © MZF

# **Ushirikiano kwenye** Elimu

**Moja ya ya maadili yetu makuu ni ushirikiano ambao msingi wake unatokana na msemo ya kiafrika usemayo “nipo sababu tupo”. Bila msaada wa asasi nyingine zinazofanya kazi kama sisi tungeweza kwenda kwa kasi lakini labda sio kwa kasi kubwa.**

Tumeingia ubia na kushirikiana na mitandao na majukwaa ambapo tunafanya kazi zenye malengo sawa. Moja wa ushirikiano ni ushiriki wetu kama wanachama wa RELI (Regional Education Learning Initiative) mtandao wenye wanachama sabini (70).

Mtandao huu unafanya kazi ya kuboresha ubora wa elimu jumuishi kwa watoto na vijana Afrika ya Mashariki. Mtandao wa RELI unasimama katika mihimili ifuatayo a; kuhakikisha mbinu inayofanya kazi na yenye ushahidi b- Kubadilisha jinsi taasisi zinavyofanya kazi na c- kushiriki kweye sera. Kupitia ubia huu tumeweza kufaidika na mbinu zinazofanya kazi na kutuwezesha kupata uwezo wa kutimiza malengo yetu. Mfano wa ushirikiano tuliouanzisha na mashirika kama Shule Direct, Uwezo, Chuo Kikuu cha Dodoma, Girls Livelihood na Mentorhsip Iniative. Ubia huu unatusaidia kutoa mafunzo kwa walimu kwenye maeneo ya elimu ya digiti, mbinu za ufundishaji lugha ya kiingereza na kutafuta ushahidi kupitia tafiti za Uwezo.



**Washiriki** wa mafunzo ya majaribio ya tathmini ya stadi za maisha. Mafunzo haya ni sehemu ya mradi wa RELI
© MZF

# AFYA YA JAMII













# Kuboresha **Huduma za Afya** Zanzibar

**Tuna lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya na kuwawezesha kuishi maisha bora makundi yaliyo kwenye hali hatarishi, na hasa wanawake na watoto.**

Malengo ambayo tumejiwekea kwenye mikakati yetu ya utoaji huduma za afya, yalibuniwa kwa ajili ya kupunguza tofauti zilizopo kati ya makundi haya yaliyo kwenye hali hatarishi na makundi mengine. Kwa hivyo, kati ya mwaka 2018 na 2021, misaada iliyotolewa na asasi yetu ililenga kwenye upatikanaji wa huduma za afya, mahitaji ya huduma za afya na uwezo wa jamii-husika katika kuzuia maradhi.

Malengo haya yangeweza tu kufanikiwa kwa njia ya kuhakikisha uwepo wa huduma za matibabu na kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuzingatia kanuni za afya bora.



Mtaalamu wa Afya katika moja ya vituo vya Afya vilivyokarabatiwa Pemba © MZF




**Pamoja na hayo**, tumekuwa tukivijengea uwezo vikundi vya wanawake hao ambao wamekua wakipata huduma katika vituo hivyo kwa kupitia vikundi vya kuweka na kukopa (VSLAs) katika masuala ya uzazi pamoja na afya ya mama na mtoto. Jumla ya vikundi 80 vya wanawake vimewezeshwa kwa njia mahsusi juu ya njia bora za kujihudumia muda mfupi kabla na baada tu ya kujifungua. Jambo la muhimu pia ni kwamba, tumekuwa tukiendesha kampeni ya kuinua kiwango cha ushirikishwaji wa wanaume katika masuala ya afya ya mama na mtoto.

Ufanisi wa juhudi zetu unaonekana ukizingatia kwamba pamekuwa na ongezeko la wenzi wa wanawake, hasa waume zao, ambao wanawasindikiza wanawake kwenda kupata huduma za wajawazito. Makundi mbalimbali ya kijamii yalishirikishwa katika kufanisha hili. Makundi haya yalikuwa ni pamoja na viongozi wa dini ambao walipata mafunzo juu ya namna ya kuwapa wafuasi wao taarifa chanya kuhusu afya ya mama na mtoto.

Kwa upande wa upatikanaji wa huduma za afya, tulielekeza macho yetu kwa tuliowaita "Vinara wa Afya" (Champions in Health) kama watu wa kujitolea katika vituo mbalimbali kwa lengo la kupunguza changamoto ya uhaba wa wataalamu wa afya.

Wengine waliopata mafunzo walikuwa wakuu wa kliniki ambao waliongezewa stadi za uongozi na utawala kwa lengo la kuongeza na kuboresha uwezo katika utoaji wa huduma za afya. Lengo hapa lilikuwa kuinua kiwango cha uridhishaji wa wateja kwenye utoaji wa huduma za afya kwa ajili ya jamii zenye uhitaji mkubwa Visiwani Zanzibar.

Miongoni mwa wanufaika wa mafunzo ya kujengea uwezo wananchi ulioendesha na asasi yetu ni Said Mtawa ambaye anatambuliwa kama kinara bora wa programu ya Vinara wa Afya. Akizungumzia uzoefu wake ndani ya proramu hii, Bw Mtawa anasema: "Nilijiunga na programu ya Vinara wa Afya nilipokuwa bado nipo chuoni (Chuo Cha Afya Mbweni) ambako niliteuliwa kuwa mmoja wa vinara wa Afya. Nimefaidika na mafunzo ya uongozi katika nyanja ya afya, nikapata nafasi ya kujitolea na kusaidia katika kuboresha afya za watu wa jamii yangu."

Akaongeza: "Ninawashukuru Milele kwa kunipatia fursa hiyo kwa sababu nilifurahia sana kufanya kazi na watu wangu ili waweze kuboresha afya zao."

Mbali na kutoa mafunzo ya uongozi, Milele iliunga mkono ukarabati wa vituo vya afya kwa lengo la kuinua utoaji huduma hasa katika eneo la masuala ya mama na mtoto.

Anasema Said: Moja ya kazi zangu ilikuwa kuhamasisha wana jamii waone umuhimu wa kwenda kupata huduma kutoka kwenye vituo vya afya na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika hili."

Akielezea sifa zake ambazo zilimwezesha afanikiwe, anasema: "Programu ya MZF ndiyo iliyoniwezesha kuinua kiwango cha hamu yangu ya kuhudumia, kujali kanuni na maadili ya kazi na weledi wa kujiwekea mipango na malengo."

Alieleza pia kuwa ufanisi wake umetokana na kuishirikisha jamii na wadau muhimu wa sekta ya afya.

Bw Said ni AfisaTabibu ambaye kwa sasa anasomea shahada ya udaktari katika Chuo Cha Kilimanjaro Christian Medical University College,Moshi.

Aidha, asasi yetu hujishughulisha na kuendeleza watoa huduma ambao si wataalamu sana wa afya ambao wana moyo wa kutoa huduma, kwa hivyo, iliandikisha waliopenda kujitolea wasaidie katika kujaza pengo la uhaba wa wafanyakazi. Zuhra Hamza Shaaban ni mmoja wa waliojitolea ambao walifanya kazi katika Kituo cha Afya cha Ukorongoni baada ya kuteuliwa na MZF.

"Kwa kuwepo kwa huduma bora za afya baada ya ukarabati na kuwekwa vifaa vilivyopatikana kwa hisani ya Milele, wanawake zaidi sasa wanapata huduma za uzazi kwenye vituo hivi .Hii ni hali ambayo haikuwahi kuonekana siku za nyuma ambapo kwenye kijiji hiki, ilikuwa ni kawaida kwa wanawake wengi kujifungulia nyumbani.."

**Said Mtawa**
Afisa tabibu katika kliniki ya MZF



**Said Mtawa**
Afisa tabibu katika kliniki ya MZF © MZF



**Zuhura Hamza Shabani**
Mfanyakazi wa kujitolea kituo cha Afya cha Ukongoroni © MZF

## Akielezea juu ya alichokipenda zaidi katika programu hii, Zuhra anasema:

"Nilifurahi sana kupata nafasi ya kufanya kazi ya kutoa huduma za afya kwa wanawake na watoto kwenye kituo... pia nilifurahia uzoefu nilioupata nilipofanya kazi maeneo ya kijijini na kuchanganyika na wanajamii katika kushughulikia changamoto za afya. Ningependa kuiomba Milele Zanzibar Foundation iendelee na programu hii na ikiwezekana, waongeze kipindi cha programu ambacho kwa sasa ni cha miezi mitatu tu."

**Zuhura Hamza Shabani**
Mfanyakazi wa kujitolea kituo cha Afya cha Ukongoroni

# **Jitihada zetu za WASH** Zaokoa Maisha

**Mipango yetu ya afya kwa muda mwingi imekuwa ikilenga katika uzuiaji magonjwa. Taasisi yetu imekuwa ikifanya juhudi za kuboresha upatikanaji maji, uondoaji wa maji-taka na usafi (WASH) kwa lengo la kupunguza hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa ya mlipuko kama vile kuharisha na yale makubwa kama huu wa sasa wa Uviko -19.**

Huduma zetu zimeunga mkono juhudi za kuongeza upatikanaji wa maji, vifaa vya uondoaji wa maji taka na kufanya usafi (WASH) katika jamii maskini Visiwani Zanzibar.

Takwimu za Shirikisho la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kwamba watu wapatao 829,000 hufa kila mwaka kutokana na ugonjwa wa kuharisha. Hii inaonyesha wazi ukubwa wa changamoto iliyopo, na hili likaleta msukumo wa haja ya MZF kutoa msaada Visiwani Zanzibar.

**Matokeo ya usaidizi wa MZF ni pamoja na haya:**




Matanki ya maji, moja ya vifaa vilivyoletwa kwa msaada wa MZF kwa ajili ya matumizi ya wanakijiji wa Kokota, Pemba.

- Kwa sasa, watu wapatao 600 katika shehia 8 Unguja na Pemba wana ufahamu wa hatua za kuboresha usafi zinazohusisha wana jamii;
- Kaya 100 zina vyoo vilivyoboreshwa kutokana na misaada iliyotolewa kwa ajili ya vifaa vya ujenzi wa vyoo.
- Hili liliwezesha kuwepo kwa vyoo bora kwa ajili ya zaidi ya watu 400 kwenye maeneo ya Bumbwini Mafufuni na Mgonjoni, Wilaya ya Kaskazini "B"
- Mabinti wapatao 650 kutoka skuli za msingi 10 walipatiwa pedi (taulo za hedhi) ambazo zinaweza kutumika zaidi ya mara moja ili waboreshe afya za "siku zao"
- Wasichana 1,000 walipatiwa vijitabu vinavyoelezea afya ya siku za hedhi, vijitabu hivi vilisambazwa kwa msaada wa MZF
- Wazazi 200 walipatiwa mafunzo juu afya ya hedhi.

# Msaada kwa **Ukarabati wa Vituo vya Afya**

Ili kuhakikisha kuna uendelevu katika utoaji bora za huduma wa afya, tulikarabati vituo vya afya ambavyo tulivijenga.

Kituo cha Afya cha Bumbwisudi,Wilaya ya Kati,Unguja kilichokarabatiwa na asasi yetu ni muhimu kwa wananchi wa eneo hili la Unguja.

Ukarabati wa kituo hiki cha afya ni muhimu kwa wakaazi wa Bumbwisudi na vijiji vya jirani. Katika mwaka wa 2020, kituo hiki kilitoa huduma kwa watu wenye uwezo mdogo wasiopungua 16,000. Idadi hii ilizidi kwa mbali na ile ambayo imepangwa ya watu 3,253.

Veronica Mateo ambaye ni mmoja wa wanufaika wa huduma ambazo zinatolewa kwenye Kituo cha Afya cha Bumbwisudi, anasema: "Huduma ambayo tumekuwa tukipata kutoka kituo hiki ni ya kiwango cha juu. Nimekuwa nikifika kituo kwa matibabu mara nyingi... wajukuu wangu pia wanakuja kutibiwa hapo. Aidha, kituo hiki kipo jirani na ninapoishi—natumia dakika 5 tu kufika kwa miguu."




Kituo cha Afya Bumbwisudi Kilichokarabatiwa na MZF © MZF



**Kiongozi Mkuu ambaye pia ni Tabibu kwenye kituo hiki, Said Fadhil Abbas,, alikuwa na haya ya kusema:**

> "Tunawashukuru sana wenzetu wa MZF kwa usaidizi wao katika kukarabati mfumo wa maji, kupiga rangi jengo zima na kuripea na kukarabati vyoo vya mashimo kwa ajili ya watu wenye ulemavu."

**Said Fadhil Abbas**
Afisa tabibu, Kituo cha Afya cha Bumbwisudi © MZF

Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo, Accelarating Progress*

# TIMU YETU



**Yousuf L. Caires**
Mwanzilishi Mwenza/Mkurugenzi Mtendaji



**Khadija Ahmed Sharrif**
Mkuu wa Miradi



**Kassim Mbarouk Juma**
Mkuu wa Uendeshaji



**Abdallah Said Abdallah**
Mkuu wa Ofisi-Pemba



**Zariha Haji Abbas**
Meneja Utawala



**Richard Komba**
Mratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini



**Alice Macmilian Mushi**
Mratibu wa Mradi -Uchumi Jamii



**Ali Bakar Amani**
Mratibu wa Mradi-Elimu



**Samson John Sitta**
Mratibu wa Mradi-Alive



**Aisha Juma Mussa**
Afisa Mradi- Elimu



**Ali Rashid**
Meneja Mradi



**Muharami Salum Issa**
Afisa Mradi-Uchumi Jamii



**Faida Kassim Omar**
Afisa Utawala



**Mhando Wazir Mhando**
Meneja Mradi-MIP



**Eshe Haji Ramadhan**
Meneja Mradi-Elimu



**Ahmada B. Haji**
Mtaalamu wa Mawasiliano



**Asha Seif Ali**
Afisa Utawala



**Salha Rashid Said**
Muhasibu Msaidizi



**Hassan Ubwa Hassan**
Afisa Manunuzi



**Said Mzee Masoud**
Dereva



**Mshauri Hassan Mussa**
Msaidizi wa Ofisi



**Shakila H. Ismail**
Afisa Mradi-Afya



**Abdilah Yahya Hassan**
Dereva



**Fatma Khamis Silima**
Afisa Mradi

Milele Zanzibar Foundation
Mbweni, P.O. BOX 933, Zanzibar
Simu: +255772229997,
Barua pepe: info@mzfn.org

**Kupata taarifa zaidi, tembelea**
www.mzfn.org

@milelezanzibarfoundation



Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo, Accelarating Progress*